

TANGAZO

NAFASI ZA AJIRA KWA DIASPORA KATIKA HOSPITALI YA AGA KHAN, DAR ES SALAAM

Ubalozi unapenda kuwatangazia kuwa Hospitali ya Aga Khan ina mahitaji ya haraka sana ya wataalamu wa Afya kuziba nafasi mbalimbali za kitabibu zilizowazi katika Hospitali hiyo. Hospitali hiyo imetoa kipaumbele kwa Watanzania wanaoishi nje ya nchi (Diaspora) kujaza nafasi hizo.

Kwa msingi wa maelezo ya hapo juu Ubalozi unawasihi Watanzania wote wenye ujuzi katika nchi za Nordic na Baltics mfikishiane taarifa hizi haraka na mchangamkie fursa hizo za ajira.

Maombi ya kazi yanatakiwa kutumwa kabla ya tarehe **8 Februari 2016** kupitia barua pepe ifuatayo; (mary.mlay@akhst.org) nakala itumwe (diaspora@nje.go.tz).

Tangazo la kazi husika limeambatanishwa kwa hatua zenu stahiki.